BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KIDATO CHA PILI (FTNA) 2015

## 015 ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA UPIMAJI WA WANAFUNZI WA KIDATO CHA PILI (FTNA) 2015

# 015 ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

Kimechapishwa na
Baraza la Mitihani la Tanzania
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2016**

Haki zote zimehifadhiwa

**YALIYOMO**

DIBAJI .......... iv

1.0 UTANGULIZI .......... 1

2.0 TATHMINI YA KILA SWALI KWA MADA .......... 2

2.1 Swali la 1: Uchaguzi wa majibu yaliyo sahihi .......... 2
2.2 Swali la 2: Ukamilishaji wa sentensi kwa kutumia maneno yaliyopo katika parandesi .......... 3
2.3 Swali la 3:Kujibu maswali kwa ufupi .......... 6
2.4 Swali la 4: Maswali ya Kuoanisha .......... 10
2.5 Swali la 5: Swala la Ijumaa na Mafunzo ya Hadithi Zilizoteuliwa .......... 12
2.6 Swali la 6: Historia ya Mitume Walioteuliwa .......... 15
2.7 Swali la 7: Zakat .......... 18
2.8 Swali la 8: Kusoma na Kuhifadhi Sura Zilizoteuliwa .......... 22

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA KILA MADA .......... 27

4.0 HITIMISHO .......... 28

5.0 MAPENDEKEZO .......... 28

Kiambatisho. .......... 30

# DIBAJI

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya Upimaji wa Kidato cha Pili 2015 kwa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, wadhibiti ubora wa elimu, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu namna wanafunzi walivyojibu maswali ya upimaji huo. Majibu ya wanafunzi katika upimaji ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha mambo ambayo wanafunzi waliweza kujifunza kwa usahihi na yale ambayo hawakuweza kujifunza kwa usahihi katika kipindi cha miaka miwili ya kwanza ya Elimu ya Sekondari.

Uchambuzi kwa kila swali umefanyika ambapo dosari mbalimbali zilizojitokeza wakati wanafunzi walipokuwa wanajibu maswali yao zimeainishwa kwa kuonesha idadi ya wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi. Uchambuzi huu umeonesha jinsi wanafunzi walivyopata alama za juu, kati na chini kwa kila swali na sampuli za majibu ya wanafunzi waliofanya vizuri au vibaya zimeoneshwa.

Taarifa hii inaonesha sababu mbalimbali ambazo zilichangia wanafunzi kuweza au kushindwa kujibu maswali kwa usahihi. Sababu zilizowafanya baadhi ya wanafunzi kuweza kujibu maswali kwa usahihi ni uelewa wa matakwa ya maswali na mada mbalimbali za somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu. Aidha, uchambuzi uliofanyika unaonesha baadhi ya wanafunzi walishindwa kujibu maswali kwa usahihi kutokana na kutotambua matakwa ya maswali na kuwa na maarifa finyu katika mada mbalimbali za somo hili. Aidha, kuna udhaifu mkubwa katika kujibu maswali ya kujieleza, kuhifadhi na kutafsiri Qur'an na Hadithi za Mtume (s.a.w).

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa mrejesho uliotolewa utawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa lengo la kupata ufumbuzi wa changamoto zilizoainishwa katika taarifa hii. Aidha, Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa endapo maoni yaliyotolewa yatafanyiwa kazi ipasavyo, ujuzi na maarifa watakayopata wanafunzi wa Kidato cha Pili katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu vitaongezeka na hatimaye kiwango cha ufaulu katika somo hili kitaongezeka.

Baraza litashukuru kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa walimu, wanafunzi na wadau wengine wa elimu kwa ujumla ambayo yatasaidia katika kuboresha taarifa ya uchambuzi wa maswali ya Upimaji wa Kidato cha Pili hasa katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu.

Mwisho Baraza la Mitihani linapenda kutoa shukrani za dhati kwa Maafisa Mitihani, Watahini, Makatibu Muhtasi na wengine wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii.



Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua ufaulu wa Upimaji wa Kidato cha Pili (FTNA) wa mwaka 2015 kwa Somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu. Upimaji wa Elimu ya Dini ya Kiislamu uliofanyika mwezi Novemba 2015 uliandaliwa kwa kuzingatia Muhtasari wa somo kwa Kidato cha I – II. Upimaji ulikuwa na sehemu A na B ambapo ulikuwa na jumla ya maswali nane. Sehemu A ilikuwa na maswali matano yenye kuhitaji majibu mafupi na ilikuwa na alama 60 na sehemu B ilikuwa na maswali matatu yaliyohitaji maelezo mafupi na ilikuwa na alama 40. Sehemu zote mbili (A na B) zilikuwa na jumla ya Alama 100.

Jumla ya wanafunzi 41,554 waliandikishwa kufanya upimaji wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu kwa mwaka 2015. Kati ya hao, wanafunzi 35,331 walifanya upimaji huu. Hii ni zaidi ya wanafunzi 914 ukilinganisha na wanafunzi 34,417 waliofanya Upimaji wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu kwa mwaka 2014. Wanafunzi 12,625 sawa na asilimia 35.74 ya wanafunzi waliofanya upimaji walifaulu ambapo asilimia 0.3 walipata A, asilimia 2.6 walipata B+, asilimia 5 walipata B, asilimia 10 walipata C na asilimia 17.8 walipata D. Wanafunzi 22,701 sawa na asilimia 64.2 walifeli ambapo asilimia 30.1 walipata E na asilimia 34.1 walipata F. Kwa ujumla ufaulu wa mwaka 2015 umeshuka kwa asilimia 12.6 ukilinganisha na ufaulu wa asilimia 48.33 wa mwaka 2014.

Taarifa hii inaonesha uchambuzi wa maswali ya upimaji na majibu yaliyotolewa na wanafunzi. Sampuli za majibu ya wanafunzi zimewekwa ili kuonesha kilichotarajiwa kufanyika na kile kilichofanywa na wanafunzi. Ufaulu wa wanafunzi kwa mada uligawanywa katika makundi matatu ya vizuri, wastani na dhaifu. Mada ilikuwa na ufaulu dhaifu kama asilimia ya wanafunzi walikuwa na alama 0 hadi 29, alama 30 hadi 49 ufaulu wake ulikuwa ni wastani na alama 50 hadi 100 ufaulu wake ulikuwa ni mzuri.

Mwisho wa taarifa limetolewa hitimisho na mapendekezo kutokana na uchambuzi wa maswali ulivyofanyika. Uchambuzi huu unatarajia kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo hili la kwa wanafunzi na hatimaye kuwa na ufaulu mzuri kwa upimaji ujao.

## 2.0 TATHMINI YA KILA SWALI KWA MADA

### 2.1 Swali la 1: Uchaguzi wa majibu yaliyo sahihi

Swali lilikuwa na vipengele vitano (i - v) na lilihusu mada za Sunnah na Hadithi, Kanuni za Usomaji wa Qur'an (Ahkaamul-Qur'an), Historia ya mitume walioteuliwa na kutayammam. wanafunzi alitakiwa kuchagua jibu sahihi kati ya majibu manne yaliyotolewa (A hadi D) na kuandika herufi yake katika kisanduku kilichowekwa. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 5, ambapo kila kipengele kati ya hivyo vipengele vitano, kilikuwa na alama 1.

Asilimia 100 ya wanafunzi waliofanya upimaji walijibu swali hili. Asilimia 5.6 ya wanafunzi walipata alama 0, asilimia 25.1 walipata alama 1, asilimia 36.1 walipata alama 2 na asilimia 33.2 walipata alama 3 hadi 5, miongoni mwao ni asilimia 1.1 tu ndio waliopata alama zote 5. Jedwali 1 linaonesha ufaulu huo kwa asilimia.

| Alama | Idadi ya Wanafunzi | Asilimia ya Wanafunzi |
|---|---|---|
| 0.0 - 1.0 | 10837 | 30.7 |
| 2.0 | 12756 | 36.1 |
| 1.0 - 5.0 | 11734 | 33.2 |
| Wasiojibu | 4 | 0.0 |
| Waliojibu | 35331 | **100.0** |

**Jedwali 1**: Ufaulu wa Wanafunzi kwa Asilimia

Kwa ujumla ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ni mzuri. Wanafunzi waliopata alama zote 5 walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika na kuelewa vipengele vya swali, hivyo kuweza kuchagua majibu kwa usahihi. Vipengele ambavyo vimejibiwa vizuri na wanafunzi wengi ni i, iv, v, ambapo wanafunzi waliweza kuchagua herufi sahihi za majibu ya vipengele hivyo. Katika kipengele cha ii na iii wanafunzi wachache (1.1%) tu ndio waliomudu kujibu kwa kuchagua herufi iliyokuwa jibu sahihi, wengi wao walishindwa. Kwa kipengele cha pili, wanafunzi wameonekana kutofahamu hukmu za Qur'an (Ahkaamul-Qur'an), hali iliyosababisha kutoelewa ni wakati gani Wau-saakin inakuwa herufi ya Madda. Katika kipengele cha (iii) kutokana na kuhusiana kwa vipotoshi na jibu, kulisababisha wanafunzi wenye uelewa mdogo wa mada kujibu kwa kuandika herufi tofauti tofauti, yaani


A, B na C. Baadhi ya wanafunzi walionekana kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu madda za Sunnah na Hadithi, Kanuni za Usomaji wa Qur'an (Ahkaamul-Qur'an), Historia ya Mitume Walioteuliwa na Kutayammam zilizotahiniwa katika swali hili na hivyo kushindwa kuchagua majibu sahihi kwa vipengele vyote vitano.

## 2.2 Swali la 2: Ukamilishaji wa sentensi kwa kutumia maneno yaliyopo katika parandesi

Swali lilihusu Mada za Sunnah na Hadithi, Tawhid, Fiqh, Qur'an na Historia ya Maswahaba wa Mtume (Al - khulafaaur – Raashidiin). Swali liliwataka wanafunzi wajaze nafasi zilizoachwa wazi katika vipengele (A - E) kwa kutumia maneno waliyopewa. Swali hili lilikuwa na alama 5 ambapo kila kipengele kilikuwa na alama 1.

Kipengele A kilipima uelewa wa wanafunzi katika Sunnah na Hadithi (uchambuzi wa Hadithi), kipengele B kilipima uwelewa wa wanafunzi katika Tawhid (kuamini vitabu vya Allah (s.w) na mitume walioshushiwa vitabu hivyo). Kipengele C kilipima uelewa wa wanafunzi katika Fiqh (nguzo ya tano ya Uislamu), kipengele D kilipima uelewa wa wanafunzi katika Qur'an na kipengele E kilipima uelewa wa wanafunzi katika Tarekh (Historia ya Uislamu baada ya Kutawafu Mtume (s.a.w).

Asilimia 100 ya wanafunzi waliofanya upimaji walijibu swali hili. Asilimia 2.1 walipata alama 0, asilimia 7.9 walipata alama 1, asilimia 19.9 walipata alama 2 na asilimia 70.1 walipata alama 3 hadi 5, miongoni mwao asilimia 13.2 walipata alama zote 5. Chati 1 inaonesha ufaulu huo kwa asilimia.




Chati 1: Muonekano wa Alama za Wanafunzi kwa Asilimia

Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ni mzuri kwani asilimia 90 ya wanafunzi waliojibu swali hili walipata alama 2-5 ambayo ndio ulikuwa ufaulu wa wastani kwa swali hili. Wanafunzi wengi waliweza kujibu vipengele vyote vitano kwa usahihi kutokana na kuwa na maarifa ya kutosha katika mada za Sunnah na Hadithi, Tawhid, Fiqh, Qur'an na Historia ya Maswahaba wa Mtume zilizotahiniwa katika swali. Pia wanafunzi wengi waliweza kuchagua maneno waliyopewa kwa usahihi kwa vipengele vyote vitano. Kielelezo 2.1 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyemudu kujibu vipengele vyote vitano kwa usahihi.

**Kielelezo 2.1**

2. Kwa kutumia maneno uliyopewa, chagua jibu sahihi ili kujaza nafasi iliyoachwa wazi katika vipengele A- E.

**Vifungu vya maneno**

| Khalifa, Injil, Ifraad, Isnad, Qiran, Imam, Zabur, Matini, Qur'an |
|---|

A Msururu wa wapokezi wa Hadithi......Isnad........................................................

B Miongoni mwa vitabu vya Allah (s.w) alichopewa Nabii issa (a.s)....Injil.......................

C Aina ya Hija ambapo Haji anavaa Ihram kwa nia ya kufanya Hija tu bila ya Umra.......Ifraad..........................................................................

D Kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake....Qur'an..........................................

E Kiongozi wa dola ya kiislamu baada ya kutawafu Mtume.........Khalifa...................

Kielelezo 2.1 kinaonesha jibu la mwanafunzi aliyeweza kujibu swali kwa kujaza majibu sahihi aliyopewa kwa vipengele vyote vitano.

Aidha, uchambuzi wa majibu ya wanafunzi umeonesha kuwa wapo wanafunzi wachache (10%) walioshindwa kujibu kwa usahihi kwa kutokuwa na uelewa wa mada za swali hili na kusababisha kutumia neno sehemu ambayo si sahihi kwa ufanano wa tahajia (herufi). Vipengele ambavyo wanafunzi hawa walivikosa sana ni cha A na C. Hii ilitokana na wanafunzi wengi kutokuwa mahiri katika mada ya Fiqh, hivyo kushindwa kujibu kwa usahihi kutokana na kutokujua uchanganuzi wa mgawanyiko wa Hadithi ambao uko katika sehemu tatu Isnad, Matin na Rawi, ujuzi ambao wanafunzi wengi waliukosa. Vile vile kwa kipengele cha C wanafunzi walihitaji kuwa na uelewa wa aina tatu za Hijja ambazo ni Ifrad, Qiran na Tamatau ili waweze kubaini ni aina gani ya hija ambapo Haji anavaa Ihram kwa nia ya kufanya Hija tu bila ya Umra. Kielelezo 2.2 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kuchagua majibu yaliyo sahihi kwa vipengele vyote vitano.

**Kielelezo 2.2**

2. Kwa kutumia maneno uliyopewa, chagua jibu sahihi ili kujaza nafasi iliyoachwa wazi katika vipengele A- E.

**Vifungu vya maneno**

| |
|---|
| Khalifa, Injil, Ifraad, Isnad, Qiran, Imam, Zabur, Matini, Qur'an |

A Msururu wa wapokezi wa Hadithi....Zabut............................

B Miongoni mwa vitabu vya Allah (s.w) alichopewa Nabii issa (a.s).......Qur an........

C Aina ya Hija ambapo Haji anavaa Ihram kwa nia ya kufanya Hija tu bila ya Umra.......khalifa..........................

D Kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake..........Imam..........................


E Kiongozi wa dola ya kiislamu baada ya kutawafu Mtume....matini.......................

Kielelezo 2.2 kinaonesha jibu la mwanafunzi ambaye aliandika majibu yasiyo sahihi kwa vipengele vyote vitano.

## 2.3 Swali la 3: Kujibu maswali kwa ufupi

Swali lilimtaka mwanafunzi kutoa majibu mafupi kwa kujaza nafasi alizopewa na lilihusu mada za Kusimamisha Swala za Sunnah, Dhana ya Dini kwa mujibu wa Qur'an, Lengo la kuumbwa mwanadamu na Historia ya mitume walioteuliwa. Swali hili lilikuwa na vipengele vitatu yaani (a), (b) na (c) na lilikuwa na jumla ya alama 20. Katika kipengele (a), wanafunzi walipimwa uelewa wao juu ya nyakati nne ambazo ni haramu, kuswali bila sababu maalum kisheria. Kipengele (b) kilikuwa na sehemu ndogo mbili; sehemu (i), kilipima uelewa wa wanafunzi juu ya maana halisi ya dini kwa mtazamo wa Qur'an, na sehemu (ii) ilipima uelewa wa wanafunzi juu ya lengo la kuletwa mwanadamu hapa ulimwenguni kwa mtazamo wa Qur-an. Kipengele (c) kilipima uelewa wa wanafunzi juu ya historia ya Nabii Ibrahim (a.s) katika mbinu alizozitumia kulingania watu wake.

Swali lilijibiwa na asilimia 99.6 ya wanafunzi wote waliofanya upimaji huu. Asilimia 10.3 ya wanafunzi walipata alama 0, asilimia 53.7 walipata alama 1 hadi 5, asilimia 23.4 walipata alama 6 hadi 9, asilimia 12.2 walipata alama 10 hadi 20 miongoni mwao ni asilimia 0.1 tu ndio waliopata alama zote 20. Hata hivyo, asilimia 0.4 ya wanafunzi waliofanya upimaji huu hawakujibu swali hili. Chati 2 inaonesha ufaulu huo kwa asilimia.




Chati 2: Muonekano wa Alama za Wanafunzi kwa Asilimia

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi umeonesha kuwa ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ni hafifu. Hii inatokana na ukweli kuwa asilimia 63.9 ya wanafunzi wote walipata chini ya alama 6. Katika kipengele (a) wanafunzi wengi walishindwa kujibu kwa usahihi kwa kuwa walitaja nyakati nne ambazo ni haramu kuswali bila ya sababu maalum kisheria. Wanafunzi wengi walishindwa kutaja mambo ambayo yakimpata mtu au yakimtokea inakuwa ni haramu kwake kuswali. Mambo hayo ni kama vile mwanamke akiwa katika hedhi (damu ya mwezi), nifasi au janaba. Katika kipengele (b) sehemu ndogo ya kwanza, wanafunzi wengi walijibu kwa mtazamo wao kinyume na maelekezo ya swali yaliyomtaka mwanafunzi kujibu kwa mtazamo wa Qur’an hivyo kueleza maana mbalimbali za dini ambazo sio sahihi. Aidha, katika kipengele (c) wanafunzi

wengi walishindwa kujaza majibu sahihi na badala yake kutaja baadhi ya mbinu alizozitumia Mtume Muhammad (s.a.w) na wengine walitaja mbinu za Nabii Nuhu (a.s) katika kulingania watu wake badala ya mbinu za Nabii Ibrahim. Zaidi ya hayo, baadhi ya wanafunzi walitaja wasifu wa Nabii Ibrahim (a.s) badala ya kutaja mbinu alizozitumia katika kulingania watu wake. Kielelezo 3.1 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.

**Kielelezo 3.1**

3. Jibu maswali yafuatayo kwa ufupi.

(a) Taja nyakati nne ambazo ni haramu kuswali bila sababu maalum kisheria.

(i) Hadithi kuoneshamani ya nafsi ya baadhi ya watu.

(ii) matini ya Hadithi haijitosheleza kimaana

(iii) wapokezi wake si katika A.S Answar.

(iv) wapokezi wake si maswahaba mashuhuri.

(b) (i) Eleza maana halisi ya dini kwa mtazamo wa Qur'an.

kukosekana maji

kuogopa wanyama wakali

ugonjwa usioruhusu kutumia maji

(ii) Kwa mtazamo wa Qur'an, nini lengo la kuletwa mwanadamu hapa ulimwenguni?

~~kw~~ kuwa safari na kukosa maji ya kutumia.

kuogopa wanyama wakali

(c) Nabii Ibrahim (a.s) alitumia mbinu sita katika kulingania watu wake. Taja mbinu tatu.

(i) hawakuuliwa hata mmoja.

walizaliwa na baba mmoja Adam ~~as~~ (a.s)

(ii) hawakuathiriwa na mazingira yao.

hawakuwahi kufanya dhambi.

Kielelezo 3.1 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi ambaye alinakili maswali mengine ya upimaji huu na kuyafanya majibu ya swali hili.

Hata hivyo, kulikuwa na wanafunzi wachache (0.1%) ambao waliweza kujibu swali hili kwa ushihi kwa vipengele vyote vitatu. Katika kipengele (a) wanafunzi hawa walitaja kwa usahihi nyakati nne ambazo ni haramu kuswali bila ya sababu maalum kisheria. Nyakati hizo ni kuswali baada ya Swala ya Alfajiri mpaka jua litakapochomoza, wakati wa kuchomoza jua, pia jua linapokuwa katikati wakati wa mchana na kuswali baada ya Swala ya Alasiri na wakati wa kuzama jua. Katika kipengele (b) wanafunzi hawa waliweza kueleza maana ya dini kwa mtazamo wa kiislamu na katika kipengele (c) waliweza kutaja mbinu tatu alizotumia Nabii Ibrahimu katika kulingania watu wake kama vile kuvunja masanamu na kujitenga mbali na familia yake. Kielelezo 3.2 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi.

**Kielelezo 3.2**

3. Jibu maswali yafuatayo kwa ufupi.

(a) Taja nyakati nne ambazo ni haramu kuswali bila sababu maalum kisheria.

(i) Wakati wa kuchomoza kwa jua

(ii) Baada ya swala ya Alasiri

(iii) Jua linapokuwa la utosi (katikati)

(iv) Baada ya swala ya Alfajiri

(b) (i) Eleza maana halisi ya dini kwa mtazamo wa Qur'an.

Dini - ni utaratibu na kanuni zinazofuatwa na mwanadamu katika maisha yake ya kila siku. hivyo hakuna asiye na dini kila mtu ana mfumo na taratibu zake

(ii) Kwa mtazamo wa Qur'an, nini lengo la kuletwa mwanadamu hapa ulimwenguni?

Kwa mtazamo wa Qur'an lengo la kuletwa mwanadamu ni kumuabudu Allah (s.w)

(c) Nabii Ibrahim (a.s) alitumia mbinu sita katika kulingania watu wake. Taja mbinu tatu.

(i) Kuvunja masanamu yaliyokuwa yakiabudiwa na makafiri.


(ii) Kujitenga mbali na familia yake kwa nia ya kulingania dini ya Allah

Kielelezo 3.2 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi vipengele vyote vitatu kwa kutaja nyakati nne ambazo ni haramu kuswali bila ya sababu kisheria, maana ya dini na sababu za kuletwa binadamu hapa dunia kwa mujibu wa Qur'an na mbinu alizotumia Nabii Ibrahimu (a.s) kulingania watu wake.

## 2.4 Swali la 4: Maswali ya Kuoanisha

Swali lilihusu mada za Tawhid, Tarekh, Fiqh, Usomaji wa Qur'an, Sunnah na Hadithi. Swali lilikuwa na vipengele 10 ambapo kila kipengele kilikuwa na alama moja 1. Swali zima lilikuwa na jumla ya alama 10 na wanafunzi walitakiwa kuoanisha vipengele vya orodha A (i - x) na vile vya orodha B (A - O) na kuandika majibu yake katika jedwali alilopewa. Vipengele katika orodha A (i na ix) vililenga kupima uelewa wa wanafunzi kuhusu Tawhid na kipengele (ii) kilipima uelewa katika Tarekh. Vipengele (iii, vi, vii, viii, na x) vilipima uelewa wa wanafunzi katika Fiqh, kipengele (iv) kilipima maarifa ya wanafunzi katika usomaji wa Qur'an kipengele (v) kilipima uelewa katika Sunnah na Hadithi.

Asilimia 99.9 ya wanafunzi wote waliofanya upimaji walijibu swali hili, ambapo asilimia 0.4 ya wanafunzi hao walipata alama 0. Asilimia 10.2 walipata alama 1 hadi 2, asilimia 33.5 walipata alama 3 hadi 4 na asilimia 55.8 walipata alama 5 hadi 10 miongoni mwao asilimia 4.5 walipata alama zote 10. Asilimia 0.1 ya wanafunzi waliofanya upimaji huu hawakujibu swali hili. Chati 3 inaonesha ufaulu huo kwa asilimia.




Chati 3: Muonekano wa Alama za Wanafunzi kwa Asilimia

Uchambuzi uliofanywa katika majibu ya wanafunzi umeonesha kuwa, ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ni mzuri kwani asilimia 89.3 ya wanafunzi walipata kuanzia alama 3. Wanafunzi wengi

(55.8%) walionekana kuwa na maarifa ya kutosha na uelewa mzuri wa kuoanisha vipengele vyote kumi (10) kwa usahihi. Kielelezo 4.1 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi vipengele vyote 10 vya swali hili.

**Kielelezo 4.1**

**MAJIBU**

| **Orodha A** | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) | (vi) | (vii) | (viii) | (ix) | (x) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Orodha B** | G | B | C | F | H | I | J | K | L | M |

Kielelezo 4.1 kinaonesha mfano wa majibu ya mwanafunzi aliyeweza kuachagua majibu sahihi kwa vipengele vyote 10 vya swali hili.

Uchambuzi zaidi katika majibu ya wanafunzi umeonesha kuwa wapo wanafunzi wachache (10.6) walioshindwa kuoanisha baadhi ya au vipengele vya swali hili. Vipengele ambavyo vilijibiwa kwa usahihi na baadhi ya hao wanafunzi ni kipengele cha (iii) ambacho jibu lake ni Tarawehe (c) na kipengele cha (vii) ambacho jibu lake ni Makka (J). Wanafunzi wengine walishindwa kuoanisha kipengele cha (i) na (ii) ambavyo majibu sahihi yalikuwa G na B. Wanafunzi ambao walishindwa kuoanisha vipengele vyote hawakuwa na uelewa mzuri wa mada za Tawhid, Tarekh, Fiqh, usomaji wa Qur'an Sunnah na Hadithi. Kielelezo 4.2 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kuoanisha kwa usahihi vipengele vyote 10 vya swali hili.

**Kielelezo 4.2**

**MAJIBU**


| **Orodha A** | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) | (vi) | (vii) | (viii) | (ix) | (x) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Orodha B** | A | G | B | F | C | I | J | H | K | L |

Kielelezo 4.2 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kuoanisha kwa usahihi vipengele vyote 10 vya swali hili.

## 2.5 Swali la 5: Swala ya Ijumaa na Mafunzo ya Hadithi Zilizoteuliwa

Swali lilihusu mada za Swala ya Ijumaa na Mafunzo ya Hadithi zilizoteuliwa na lilikuwa na vipengele viwili (a) na (b) ambapo kipengele (a) kilikuwa na alama (5) na kipengele (b) kilikuwa na alama (15) na kufanya swali hili kuwa na jumla ya alama (20). Kipengele (a) katika swali hili kililenga kupima uelewa wa wanafunzi katika Swala ya Ijumaa. Wanafunzi walipewa nguzo tano za khutba ya Ijumaa (maelezo) zilizochanganywa utaratibu wake na kutakiwa wazipange nguzo hizo katika mtiririko ulio sahihi. Katika kipengele (b) wanafunzi walipimwa uhifadhi wa Hadithi za Mtume (s.a.w) na uwezo wake wa kuelezea mafunzo yanayopatikana katika Hadithi hizo. Swali lilinukuu Hadithi ya Mtume (s.a.w) iliyobainisha kuwa Allah (s.w) hatazami viwiliwili vya waja, wala hatazami sura zao, lakini hutazama katika nyoyo zao. Mwanafunzi alitakiwa kumtaja swahaba aliyepokea Hadithi hii na aliyeiandika na kisha kueleza mafunzo matatu yatokanayo na Hadithi hiyo.


Swali lilijibiwa na Asilimia 99.9 ya wanafunzi wote waliofanya upimaji huu. Asilimia 12.7 ya wanafunzi waliofanya swali hili walipata alama 0, asilimia 65.2 walipata alama 1 hadi 5, asilimia 16.5 walipata alama 6 hadi 9, asilimia 5.6 walipata alama 10 hadi 20. Asilimia 0.1 ya wanafunzi waliofanya upimaji huu hawakujibu swali hili. Chati 4 inaonesha ufaulu huo kwa asilimia.




Chati 4: Muonekano wa Alama za Wanafunzi kwa Asilimia.

Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ni hafifu. Hii inatokana na ukweli kuwa wanafunzi wengi (87.3) hawakuweza kujibu kwa usahihi vipengele vyote vya (a) na (b). Wanafunzi hao walishindwa kupanga maelezo ya nguzo tano za Swala ya Ijumaa zilizovurugwa katika mtiririko sahihi katika kipengele (a). Pia wanafunzi hao walionekana kuwa na maarifa madogo katika mada ya Fiqh na Swala ya ijumaa kwa ujumla na hivyo kushindwa kubaini mpangilio sahihi wa nguzo za Khutba ya Ijumaa. Katika kipengele (b) wanafunzi hao walishindwa kujibu vipengele vya Hadithi walivyoulizwa. Hii ilitokana na wanafunzi kukosa maarifa na umahiri na ujuzi katika mada ya Sunnah na Hadithi hivyo kushindwa kutaja mwandishi na mpokezi wa Hadithi waliyopewa pamoja na mafunzo ya Hadithi hiyo. Kwa mfano, wanafunzi wengi walimtaja Abuu Daud kuwa ni mpokezi wa Hadithi badala ya Abu Hurayra ambaye ndiye mpokezi sahihi. Ufaulu hafifu wa wanafunzi katika kipengele (b) ulitokana na wanafunzi kukosa maarifa katika kuhifadhi Hadithi za Mtume (s.a.w) na uwezo wa kutoa mafunzo ya Hadithi hiyo. Kielelezo 5.2 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi:-

**Kielelezo 5.2**


MAJIBU

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
|---|---|---|---|---|
| A | E | C | B | D |

(b) Mtume (s.a.w) amesema "Kwa hakika Allah hatazami viwiliwili vyenu wala sura zenu, lakini anatazama nyoyo zenu".

(i) Nani aliyepokea Hadithi hiyo? Aliyepokea hadithi hii ni Bokar wa [illegible]

(ii) Taja aliyeandika Hadithi hiyo... Alio andika hadithi hii ni Abuuhurayra (r.a)

(iii) Eleza mafunzo matatu yatokanayo na Hadithi hiyo.

i) Inatufundisha tuache majivuno

ii) Hadithi hii inatufundisha roho nzuri

iii) Hadithi hii inatufundisha kuwa na imani pindi tunapo [illegible] kaaniwa.

Kielelezo 5.2 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi ambaye alishindwa kupanga vipengele vya khutba vilivyochanganywa katika mtiririko ulio sahihi na pia kutaja mpokeaji na mwandishi wa Hadithi na kueleza mafunzo matatu yatokanayo na Hadithi hiyo.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa Wanafunzi wachache (12.7%) waliweza kujibu swali hili kwa usahahi. Katika kipengele (a) wanafunzi hao waliweza kupanga katika mtiririko ulio sahihi nguzo tano za Swala ya Ijumaa. Hii inatokana na Swala ya Ijumaa kuswaliwa mara moja kila wiki kwa Waislamu wote hivyo kuwawezesha wanafunzi kukumbuka kwa urahisi mpangilio wa nguzo za khutba ya Ijumaa. Katika kipengele (b) wanafunzi wachache waliweza kujibu kwa usahihi kwa kutaja mpokeaji na mwandishi wa Hadithi na pia kueleza mafunzo matatu yatokanayo na Hadithi hiyo. Kielelezo 5.1 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi.

**Kielelezo 5.1**

**MAJIBU**

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
|---|---|---|---|---|
| D | C | E | A | B |

(b) Mtume (s.a.w) amesema "Kwa hakika Allah hatazami viwiliwili vyenu wala sura zenu, lakini anatazama nyoyo zenu".

(i) Nani aliyepokea Hadithi hiyo? Abu Huraira

(ii) Taja aliyeandika Hadithi hiyo Muslim

(iii) Eleza mafunzo matatu yatokanayo na Hadithi hiyo.

a- Allah hamhukumu mtu kwa kuringalia sura yake (tajiri au maskini) (Muarabu au muajemi)

b- Allah humhukumu mtu kwa matendo yake aliyoyafanya duniani (Mabaya au mema)


c- Moyo ndio kila kitu katika mwili na maisha ya mwanadamu (pindi utakapotakasika basi mwili mzima utakuwa msafi na endapo utachafuka basi mwili mzima utakuwa mchafu) na ndio maana ~~Alla~~ Allah huangalia nyoyo za watu

Kielelezo 5.1 kinaonesha jibu la mwanafunzi ambaye aliweza kupanga vipengele vya khutba vilivyochanganywa katika mtiririko ulio sahihi na pia kutaja mpokeaji na mwandishi wa Hadithi na kueleza mafunzo matatu yatokanayo na Hadithi hiyo.

## 2.6 Swali la 6: Historia ya Mitume Walioteuliwa

Swali hili lilihusu mada ya Historia ya mitume walioteuliwa. Swali lililenga kupima ujuzi walionao wanafunzi katika kueleza sababu tano zilizosababisha Bani Israil kulaaniwa na Allah (s.w). Swali hili lilikuwa na alama 10, ambapo mwanafunzi alitakiwa kupata alama mbili (2) kwa kila sababu aliyoieleza vizuri.

Asilimia 89.6 ya wanafunzi wote waliofanya upimaji huu walijibu swali hili, ambapo asilimia 49.6 ya wanafunzi hao walipata alama 0. Asilimia 9.9 walipata alama 1 hadi 2, asilimia 8.4 walipata alama 3 hadi 4 na asilimia 21.7 walipata alama 5 hadi 10 ambapo asilimia 8.4 miongoni mwao walimudu kupata alama zote 10. Hata hivyo asilimia 10.4 ya wanafunzi waliofanya upimaji huu hawakujibu swali hili. Chati 5 inaonesha ufaulu huo kwa asilimia.




Chati 5: Muonekano wa Alama za Wanafunzi kwa Asilimia

Uchambuzi uliofanywa katika majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa baadhi ya wanafunzi (8.4%) waliweza kujibu swali hili vizuri na kupata alama za juu. Wanafunzi hao walieleza sababu tano za "Banu Israil" kulaaniwa na Allah (s.w). Sababu hizo ni kukaidi amri za Allah (s.w), kuwa wezi wa fadhila, kukadhibisha na kuuwa mitume wa Allah (s.w) na kuvunja ahadi ya Allah (s.w). Kielelezo 6.2 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyejibu swali hili kwa usahihi.

**Kielelzo 6.2**

6. Eleza sababu tano zilizosababisha Bani israil kulaaniwa na Allah (s.w).

(i) Walikuwa ni wezi wa fadhila Bani israel waliijaliwa neema za aina mbalimbali katika eneo lao lakini hawakuwa ni wenye kumshukuru Allah s.w

(ii) Walikuwa wakichanganya haki na batili. Tatizo mojawapo pia la kulaaniwa kwa bani israil ni kwamba walikuwa ni wenye kuchanga vyote vitendo vizuri na vibaya vyote waliviona sawa tu.

(iii) Walikuwa wakiwaua mitume. Pia tukio lingine la kusikitisha kwa bani Israil ni lile la kuwaua mitume mbalimbali ya Allah s.w hali ya kuwa kutokana na kuleta ujumbe kwao

(iv) Walikuwa wakiamrisha kufanya mema hali ya kuwa wao hawafanyi mema wanafanya maovu; Pia bani Israil katika tukio mojawapo la kusikitisha na kumkera Allah kwa kuamrishana mema hali ya kuwa wakifanya kinyume chake.

(v) Walikuwa wepu wakikufuru na kukadhibisha dini; Hii inathibitishika pale watu wachache walipomwambia nabii Musa (a.s) hali wanataka kumuona Allah (wanataka kwenda mbinguni)

Kielelezo 6.2 kinaonesha jibu la mwanafunzi ambaye aliyeeleza sababu tano zilizosababisha Bani Israil kulaaniwa na Allah (s.w).

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wastani. Chati inaonesha kuwa asilimia 59.5 ya wanafunzi waliojibu swali hili walishindwa kupata alama 3 ambayo ilikuwa ni ufaulu wa wastani kwa swali hili. Wanafunzi wengi (49.8%) waliopata alama 0 hadi alama 1 hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada ya Historia ya

mitume walioteuliwa hivyo kushindwa kueleza sababu zilizosababisha Bani Israil kulaaniwa na Allah (s.w). Aidha, wanafunzi hao walishindwa kujibu swali hili kutokana na kushindwa kuelewa maana ya neno "Bani Israil" lililomo ndani ya swali. Kuna ambao walijibu swali hili kwa dhana ya neno "Bani Israil" ni Malaika na ambao walijibu kwa dhana ya Firaun na pia waliojibu kwa dhana ya maana ya Iblisi ambayo yote hayakuwa majibu sahihi. Kielelezo 6.1 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.

**Kielelezo 6.1**

6. Eleza sababu tano zilizosababisha Bani israil kulaaniwa na Allah (s.w).

(i) Bani Israil alikua anajitangazia yeye ndiye Mwenyezimungu Bani Israil alikua akijitangaza kuwa yeye ni Allah <s.w> na wahu wote wamuabudu yeye peke yake

(ii) Alikua anataka binadamu wote wamnyenyekee yeye Bani Israil alitaka viumbe wengine au wanadamu wote wamtukuze yeye kama mungu wao aliyewaumba wamsujudie wakati anayetakiwa kunyenyekewa ni Allah <s.w> peke yake

(iii) Hakutaka kumuabudu mola wake aliyemuumba Bani Israil alikataa kata kata kumuabudu Allah <s.w> kwa sababu alisema hamna mungu zaidi yake kwa hiyo hakumuabudu Allah <s.w> na alifanya kinyume na Ibada za Allah

(iv) Kumshirikisha Allah <s.w> Bani Israil alikua akifanya ushirikina kwa kumshirikisha Allah alikuwa akidanganya wahu kwamba hakuna mungu kama yeye


(v) Kufanya mambo kinyume na Allah <s.w> bani ~~H~~ Israil alikua akifanya mambo kinyume na Allah <s.w> ambayo anataka mungu akitaka hiki yeye anafanya kile

Kielelezo 6.1 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi alieleza sababu za Israil (mtu/firauni) kulaaniwa na Allah badala ya kuandika sababu zilizosababisha Bani Israil (watu) kulaaniwa na Allah (s.w).

## 2.7 Swali la 7: Zakat

Swali liligawanyika katika vipengele viwili (a) na (b) na lilihusu mada ya Zakat. Kipengele (a) katika swali hili kililenga kupima uelewa wa mwanafunzi juu ya maana ya Zakat kisheria. Kipengele (b) kilimtaka mwanafunzi aeleze masharti matano ya kuzingatia katika ukamilifu wa utoaji wa Zakat. Swali lilibeba jumla ya alama (15), ambapo kipengele (a) kilikuwa na alama tano (5) na kipengele (b) kilikuwa na alama (10).

Swali lilijibiwa na asilimia 97.4 ya wanafunzi wote waliofanya upimaji huu. Asilimia 44.1 ya wanafunzi wote waliojibu swali hili walipata alama 0, asilimia 35 walipata alama 1 hadi alama 4; asilimia 8 walipata alama 5 hadi 7, asilimia 10.3 walipata alama 8 hadi 15, miongoni mwao asilimia 0.2 tu ndio waliomudu kupata alama zote 15. Hata hivyo asilimia 2.6 ya wanafunzi waliofanya upimaji huu hawakujibu swali hili. Chati 6 inaonesha ufaulu huo kwa asilimia.




Chati 6: Muonekano wa Alama za Wanafunzi kwa Asilimia

Uchambuzi katika majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ni hafifu kwani asilimia 79.1 ya wanafunzi wote waliojibu swali hili walipata chini ya alama 5. Miongoni mwao, asilimia 44.1 walipata alama 0. Baadhi ya wanafunzi hao waliacha kujibu swali hili hasa kipengele (b) na wengine kuandika majibu kinyume na matakwa ya swali. Aidha, majibu mengi walioandika wanafunzi hao yalijikita katika kiwango

cha zakat, muda wa zakat na wanaostahili kupewa zakat, majibu ambayo hayakuwa sahihi. Hali hii inaonesha kuwa wanafunzi hawakuwa na uelewa mzuri wa mada ya Zakat na hivyo kushindwa kueleza masharti matano ya kuzingatia katika utoaji wa Zakat. Wanafunzi wachache walioleza masharti ya Zakat yalikuwa pungufu ya matano hivyo kupata alama za chini. Kielelezo 7.1 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi.

**Kielelezo 7.1**

7. (a) Eleza maana ya Zakat kisheria.

Nizakatat ingo iuzu kutolewa na mtu mpaka ifikie kiwango cha kee maalum au kufikia nisaab nakufikia sehemu ingpo stahiki n.k

(b) Eleza masharti matano ya kuzingatia ili ibada ya utoaji Zakat ikamilike.

(i) zakat hutolewa kwa mtumwenye mali tu au tajiri zakat hutolewa na mtu ambae mwenye uwezo mkubwa wa kutoa hutolewa fedha nakituchochote ili ibada ikamilike zakat haina kiwango zakat tofauti na swadaq.

(ii) zakat hutolewa ili kufika kiwango cha kinachotaka kiwa hutolewa mpaka ifikie nisaab zakat haitolewi madada wowote wala zakat haina kiwango cha kutoa zakat inatolewa kwamtu mwenye fedha na tajiri

(iii) zakat hutolewa kwa muislamu na kupewa mtu mbae ana uwezo au ana kitu cha kujihudumia na pia vile vile zakat hutolewa kwa mtu tajiri zakat hutolewa ili mpaka ibada ya swala ikamilike

(iv) zakat haina kiwango cha kutoa zakat tofauti na swadaq zakat hutolewa ilikujikisha kiwango kinacho takiwa zakat ni mali inayo jua kutolewa muislamu na zakat ni kama ibada kwa sababu kila unapotoa unaandikiwa swawabu.

(v) zakat haitolewi wakati wowote na mdawowote zakat ni mali au Fedha, vito zakat ni mtu tajiri ndo atoe kama ni mazao yote ya shambani wanyama wa fugwao zakat ni ukitoa sawa na ibada zakat nguzo

Kielelezo 7.1 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeeleza sababu za kutolewa Zakat badala ya masharti matano ya kuzingatia katika utoaji wa Zakat.

Wanafunzi wachache sana (0.2%) waliweza kujibu kwa usahihi na kueleza maana ya Zakat kisheria kuwa ni sehemu ya mali ya tajiri, anayoitoa kwa kutekeleza amri ya Allah (s.w), kuwapa wanaostahiki, baada ya kupindukia mwaka au mavuno iwapo mali hiyo imefika nisab. Katika kipengele (b), wanafunzi hao walieleza masharti ya utoaji wa Zakat ambayo ni kutoa vilivyo halali, kutoa vilivyo vizuri, kutoa kati na kati, kujiepusha na riyaa na kutofuatilia na masimbulizi baada ya kutoa na kuwapa wanaostahiki Kielelezo 7.2 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyejibu kwa kufuata matakwa ya swali. Kielelezo 7.2 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi.

**Kielelezo 7.2**

7. (a) Eleza maana ya Zakat kisheria.

Ni mali ya tajiri iliyofikia nisabu inayojuzu kutolewa ~~zakkah~~ zakat kupewa wanaostahiki baada ya kupindukia mwaka au baada ya Mavuno.

(b) Eleza masharti matano ya kuzingatia ili ibada ya utoaji Zakat ikamilike.

(i) kutoa uliiyo halali; katika utoaji wa zakkah mtu anatakiwa atoe uliiyo halali na pindi atakapotoa iliyo haramu sawa sawa na hajatoa kitu, kwani uislamu umeharamisha vitu vya haramu.

(ii) kutoa uliiyo vizuri; Pia vile vile miongoni mwa sharti la zakat kutoa uliiyo vizuri. kwani mtume anasema mpendelee muislamu mwenzako kama unavyopenda nafsi yako. Hivyo kama waislamu inabidi tutoe uliiyo vizuri

(iii) Kutoa kati na kati: hii inaangalia kuwa katika matumizi yako unatumia kiasi gani cha chakula mfano: Mchele, hiyo ndiyo utakubidi utoe katika.

(iv) kujiepusha na riya na masimbulizi: yule mtoaji wa zakat anatakiwa ajiepushe na kujionesha kuamba yeye ndiye katoa zakat kama wengine wanavyo kwenye matuvi siku hizi wanajionesha sana


(v) Kuwapa wanaostahiki: katika utoaji wa zakat katika kugawa hiyo mali kuna watu ambao wanastahiki mfano: Mafukara, Maskini, Wanaotumikia, watumwa wa nguvu nyoyo zao, kuwakomboa yatima, waliohamakika na safari, Mtoto wa njia.

Kielelezo 7.2 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyemudu kueleza maana ya Zakati kisheria na pia masharti matano ya kuzingatia katika ukamilifu wa utoaji wa Zakat.

## 2.8 Swali la 8: Kusoma na Kuhifadhi Sura Zilizoteuliwa

Swali lilihusu mada ya Kusoma na Kuhifadhi Sura Zilizoteuliwa na lililenga kupima uhifadhi na uzingatiaji wa mafunzo yatokanayo na aya za Qur-an. Swali liligawanyika katika vipengele viwili (a) na (b). Kipengele (a) kilimtaka mwanafunzi aandike tafsiri ya Suratul Fat-ha na kipengele (b) kilimtaka mwanafunzi atoe maelezo kuhusu walioneemeshwa, walioghadhibikiwa na Allah (s.w), na waliopotea. Kipengele (a) kilikuwa na alama (6) na kipengele (b) kilikuwa na alama 9, jumla alama 15.

Swali lilijibiwa na asilimia 95.2 ya wanafunzi wote waliofanya upimaji huu. Asilimia 19.2 ya wanafunzi wote waliojibu swali hili walipata alama 0, asilimia 36.9 walipata alama 1 hadi 4; asilimia 24.4 walipata alama 5 hadi 7, asilimia 14.7 walipata alama 8 hadi 15, miongoni mwao asilimia 0.2 tu ndio waliomudu kupata alama zote 15 za swali hili. Asilimia 4.8 ya wanafunzi waliofanya upimaji huu hawakujibu swali hili. Chati 7 inaonesha ufaulu huo kwa asilimia.



Chati 7: Muonekano wa Alama za Wanafunzi kwa Asilimia

Baadhi ya wanafunzi waliweza kujibu swali hili kwa usahihi kwa kutafsiri aya zote sita vizuri na kutoa maelezo sahihi yanayohusu watu walioneemeshwa, walioghadhibikiwa na Allah (s.w) na waliopotea. Wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kutosha na uelewa wa mada ya Sura zilizoteuliwa. Aidha, waliweza kutoa tafsiri sahihi ya Suratul-Fat-ha kuwa, Kwa jina la mwenyezi Mungu, mwingi wa rehma mwenye kurehemu, sifa zote zinamstahikia Allah Bwana na mlezi wa viumbe vyote, mwingi wa rehma, mwenye kurehemu, mwenye kumiliki siku ya malipo wewe tu ndiye tunayekuabudu na wewe tu ndiye tunayekuomba msaada, tuongoze katika njia iliyonyooka, njia ya wale uliowaneemesha, sio ya wale waliokasirikiwa, wala ya wale waliopotea. Wanafunzi hao walieleza kuwa watu walioneemeshwa ni wale waliojitahidi kuendesha maisha yao kwa kufuata kanuni na sheria za Allah (s.w) na kujitoa muhanga ili kuufanya Uislamu utawale. Aidha, waliweza kufafanua kuwa walioghadhibikiwa na Allah (s.w) ni mayahudi ambao baada ya kujua ujumbe wa Allah (s.w) hawakuufuata inavyotakikana na kuamua kufuata baadhi ya mwongozo na kukanusha mwingine. Waliopotea ni wale washirikina na manaswara ambao pamoja na kudai kuwa wanamuamini Mwenyezi Mungu hawakufuata mwongozo wake kwa kutii kanuni zake zote. Kielelezo 8.2 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi kama ilivyopaswa.

**Kielelezo 8.2**

8. (a) Andika tafsiri ya Suratil-Fat-ha

(i) Kwajina la mwenyezimungu, mwingi wa rehma, mwenye kurehemu kila sifa njema anastahiki mwenyeng'ezimungu mlezi wa viumbe vyote ni mola wetu mmoja tu wakusujudia na yeye ni mlezi wetu wote

(ii) Mwingi wa rehma, mwenye kurehemu, mwenye kunee mesha neema kubwa na mwenye kuneemesha neema ndogo ni mwenye kuneemesha neema

(iii) Mwenye kumiliki, siku ya malipo, mwenye kuhesabu neema za watu wa peponi na mwenye kuhesabu na uvo ya watu wa motoni ni siku ambayo watu wa peponi wata enda kwao na wa peponi wata enda kwao

(iv) wewetu mwenyeng'ezimungu tunaye kuabudu, na wewetu mwenyeng'zimungu tunaye kuomba msaada / msamaha ili utuongoze katika watu ambao umewakaririkia

(v) Tuongoze katika njia iliyonyooka

(vi) Njia ya wale uliyowaneemesha juu yao, wala sio ya wale uliowakasirikia juu yao, wala sio ya wale waliopotea.

(b) Kwa mujibu wa Suratil-Fat-ha toa maelezo kuhusu watu wafuatao:

(i) Walioneemeshwa kwa mujibu wa Qur-an (suratil-fatha walioneemeshwa ~~na~~ ni wale Mitume, Manabii, watu wemanawachamungu

(ii) Walioghadhibikiwa na Allah (s.w).

Walioghabhibikiwa ni mayahaudi kwa sababu wanaijua haki na wanakataa kuifuata, ndiyo sababu ya kukasirikiwa na Allah

(iii) Waliopotea.

Hawa ni wale manaswara ambao wanafanya ibada ambayo hawaijui mfano: wanaiyo mualud nabii ~~musa~~ issa na kumuita Mungu. Hivi ndiyo maana ~~wanasema~~ tunasema wamepotea.

Kielelezo 8.2 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeweza kuandika tafsiri ya suratul Fat-ha na kutoa maelezo kuhusu walioneemeshwa, walioghadhibikiwa na Allah (s.w) na waliopotea.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wastani kwani asilimia 56.1 walipata alama chini ya 5 ambayo ni alama ya ufaulu wa wastani. Ufaulu wastani katika swali hili ulitokana na uhifadhi duni wa Qur'an waliokuwa nao wanafunzi hususan wa sura zilizoteuliwa. Aidha, wanafunzi wengi walishindwa kutoa tafsiri ya Suratul Fat-ha kwa usahihi ambapo kumetokana na kutoweza kubainisha mafunzo yatokanayo na sura hii. Wanafunzi walioweza kutafsiri aya za

Suratul Fat-ha, baadhi yao walishindwa kubainisha mafunzo ya Sura hiyo na hivyo kupata alama za chini. Wapo wanafunzi walioshindwa kabisa kuandika tafsiri ya Sura hiyo pamoja na mafunzo yake na kuacha wazi nafasi ya kujibia waliyopewa. Sehemu ya kuelezea mafunzo iliachwa wazi kabisa au wanafunzi waliandika neno moja badala ya kueleza mafunzo kama swali lilivyo wataka. Hali hii inadhihirisha uwezo mdogo wa wanafunzi wengi katika kujibu maswali ya kujieleza. Kielelezo 8.1 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.

**Kielelezo 8.1**

8. (a) Andika tafsiri ya Suratil-Fat-ha

(i) Walioneemeshwa na allah (s.w) ni kitendo cha kupewa neema mdogo ndogo na kubwa kubwa na Allah (s.w)

(ii) Walio ghadhibikiwa na Allah (s.w). Ni kitendo cha kumkasilisha Allah (s.w)

(iii) Walio potea Ni kitendo cha kutomchamungu allah (s.w)

(iv) Walio staarabishwa ni watu kuwa na adabu na kusikiliza mtu maneno anayomweleza na

kuyatii matakwa anayo ambiwa

(v) Kurakinishwa na Allah (s.w) kitendo cha kurikiliza mtu na kuelewa Allah (s.w) nini anacho kuhitaji

(vi) Kuabudiwa kwa Allah (s.w) watu kuwa na Uchamungu wa kumuomba mola wao awajalie neema na baraka za Allah (s.w)

(b) Kwa mujibu wa Suratil-Fat-ha toa maelezo kuhusu watu wafuatao:

(i) Walioneemeshwa ni watu ambao walio pewa ridhiki ndogo ndogo na kubwa kubwa

(ii) Walioghadhibikiwa na Allah (s.w).

ni watu ambao walikasirikiwa na Allah (s.w) kwa sababu walimuudhi na kuto mtii asema cho Allah (s.w)

(iii) Waliopotea.

watu ambao walipotea katika imani ya kiislamu na kwenda kuabudu midana mu

Kielelezo 8.1 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeeleza maana isiyo sahihi ya maneno mbalimbali badala ya kuandika tafsiri ya suratul Fat-ha na kutoa maelezo kuhusu walioneemeshwa, walioghadhibikiwa na Allah (s.w) na waliopotea.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA KILA MADA

Uchambuzi uliofanyika kwa kuangalia majibu ya wanafunzi umeonesha kuwa wanafunzi walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada za *Sunnah na Hadithi, Tawhid, Fiqh, Historia ya Maswahaba wa Mtume (Al-khulafaaur – Raashidiin), Kanuni za Usomaji wa Qur'an (Ahkaamul-Qur-an), na kutayammam.* Hata hivyo, Wanafunzi wachache walikuwa na uelewa mdogo wa mada ya *Swala ya Ijumaa, Mafunzo ya Hadithi zilizoteuliwa na Zakat*. Baadhi ya Wanafunzi kutojibu kabisa baadhi ya vipengele vya maswali hasa ya kujieleza (swali la 7 na 8), kuandika majibu yasiyoendana na matakwa ya swali, kutoa majibu yasiyo sahihi hasa katika maswali ya kuchagua na kuoanisha, ni dalili tosha kuwa hawakuzingatia mafunzo katika muhtasari wao, walikuwa na maandalizi duni au mada nyingi zilizotahiniwa hawakuzielewa ipasavyo. Mada iliyofanyika vizuri ni mada ya *Sunnah na Hadithi* ambayo ilikuwa na ufaulu wa asilimia tisini (90%). Mada iliyofanyika vibaya ni mada ya *Zakat* ambayo ilikuwa na ufaulu wa asilimia ishirini (20%) wakati mada iliyo na ufaulu wa wastani

ilikuwa mada ya *Historia ya Mitume Walioteuliwa* ambayo ilikuwa na asilimia 40.5.

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa ufaulu wa wanafunzi kwa kila swali umewasilishwa katika makundi makuu matatu ambapo waliopata alama kati ya 0 hadi 29 ufaulu wao ni hafifu na umewakilishwa na rangi nyekundu kwenye jedwali. Wanafunzi waliopata alama kati ya 30 hadi 49 ufaulu ni wa wastani ambao umewakilishwa na rangi ya njano kwenye jedwali na waliopata kati ya alama 50 hadi 100 ufaulu ni mzuri ambao kwenye jedwali umewakilishwa na rangi ya kijani (rejea kiambatisho).

Kwa ujumla ufaulu wa wanafunzi katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu mwaka 2015 kwa Kidato cha Pili ni mzuri. Hii ilitokana na wanafunzi kufaulu vizuri katika swali la 1 lilohusu mada za *Sunnah na Hadithi*, *Kanuni za Usomaji wa Qur'an (Ahkaamul-Qur-an), Historia ya mitume walioteuliwa na kutayammam,* swali la 2 lililokuwa na mada za *Sunnah na Hadithi, Tawhid, Fiqh, Qur'an Historia ya maswahaba wa Mtume (Al-khulafaaur – Raashidiin)* na swali la 4 lililokuwa na *mada za Tawhid, Tarekh, Fiqh, Usomaji wa Qur'an* na *Sunnah na Hadithi*. Wanafunzi hawakufanya vizuri katika swali la 5 lililokuwa na mada za Swala ya *Ijumaa na Mafunzo ya Hadithi* zilizoteuliwa na swali la 7 lililokuwa na mada ya *Zakat.*

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha ufaulu katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu yafuatayo yanaweza kusaidia kuleta mabadiliko:

(a) Walimu wafundishe na kumaliza mada zote katika muhtasari ili kutoa fursa kwa wanafunzi kujiandaa kikamilifu kukabiliana na swali lolote kutoka katika muhtasari wao.

(b) Wanafunzi wajengewe tabia ya kujisomea vitabu vya kiada na ziada vya Elimu ya Dini ya Kiislamu ili kuwaandaa kwa mujibu wa muhtasari na kuwawezesha kuwa na maarifa ya kutosha kujibu maswali hasa ya kujieleza.

(c) Katika mada ya Qur'an wanafunzi watiliwe mkazo kuweza kutafsiri

sura zilizoteuliwa na kubainisha mafunzo ya sura hizo.

(d) Pamoja na sura zilizochaguliwa, ni muhimu wanafunzi wajengewe tabia ya kuisoma Qur'an nzima mara kwa mara ili kujiwekea msingi imara wa Elimu ya dini.

(e) Wanafunzi wapewe mazoezi mengi na ya aina mbalimbali ili kuwajengea umahiri wa kutambua matakwa ya swali na uwezo wa kuibua majibu sahihi.

**Kiambatisho.**

**UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KIMADA NA KWA ASILIMIA**

| S/N | Mada | Nambari ya Swali | Asilimia ya Wanafunzi Waliopata Alama 30 au Zaidi | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Sunnah na Hadithi, Tawhid, Fiqh, Qur'an na Historia ya Maswahaba wa Mtume (Al-khulafaaur – Raashidiin). | 2 | 90 | Vizuri |
| 2 | Tawhid, Tarekh, Fiqh, usomaji wa Qur'an, Sunnah na Hadithi. | 4 | 89.4 | Vizuri |
| 3 | Sunnah na Hadithi, Kanuni za Usomaji wa Qur'an (Ahkaamul-Qur-an), Historia ya mitume walioteuliwa na kutayammam. | 1 | 60.3 | Vizuri |
| 4 | Kusoma na kuhifadhi Sura zilizoteuliwa. | 8 | 43.9 | Wastani |
| 5 | Historia ya Mitume walioteuliwa. | 6 | 40.5 | Wastani |
| 6 | Kusimamisha Swala za Sunnah, Dhana ya Dini kwa mujibu wa Qur'an, Lengo la kuumbwa mwanadamu, na Historia ya Mitume walioteuliwa. | 3 | 36.1 | Wastani |
| 7 | Swala ya Ijumaa na Mafunzo ya Hadithi zilizoteuliwa. | 5 | 22.1 | Hafifu |
| 8 | Zakat. | 7 | 20.8 | Hafifu |
| | Wastani wa Jumla | | 50.4 | Mzuri |